



Katika mji fulani, kulikuwa na duka nadhifu la viatu vya bei ghali.

Ni katika mji huu ndimo nilizaliwa.



Watu wengi walikuja  
kwenye duka hilo la viatu,  
lakini ni wachache tu  
walioweza kununua viatu  
hivyo vya mapambo.

Siku moja, mwanamume  
tajiri mwenye miguu  
mikubwa alilitembelea  
duka lile.



Alizeweke pesa zake  
kwenye kaunta.

Kisha, akiwa ameiweka  
mikono yake mifukoni,  
alitembea juu na chini  
akiviangalia viatu.



Aliponikaribia, nilikosa  
pumzi na kuganda.

Aliinyosha mikono yake na  
kunikamata.

Aliketi na kuanza kunivaa  
kwenye miguu.



Alikuwa na miguu  
mikubwa, na harufu  
ilikaribia kunikosesha  
pumzi!

Nilipakiwa kwenye  
sanduku.

Tulienda nyumbani,  
akaniweka kwenye kabati.



Alinivaa kila siku.

Nilimfanya akawa nadhifu  
na akatembea kwa ujasiri.

Nilikuwa na maisha  
magumu. Kwa kuwa  
alikuwa mvivu, hakuiosha  
miguu yake!



Kwa upande wangu,  
nilimng'ata wakati  
mwingine, na kumfanya  
achechemee.

Mwishowe, nilizeeka na  
kuvunjika, nikawa na  
makovu na nyufa.

Aliniweka nje, karibu na  
pipa la takataka.



Mtu mwingine alinipeleka  
kwenye karakana ya ngozi  
ili nichakatwe.

Huko, nilitengenezwa  
mkoba mpya  
uliometameta.

Nilianza maisha mapya.